JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

SHULE YA SEKONDARI MAKITA,
S.L.P 455,
**MBINGA.**

TAREHE: ………………..

***Simu Na. 025 – 2640531***
***Mkuu wa shule: 0755480158***
***Makamu Mkuu wa Shule:076579272***
***Makamu mkuu wa shule taaluma;0752494883***
***KUMB.NA.MKTSS/WNFN/ADM/F5/2023.***
JINA LA MWANFUNZI: ……………..
……………………………..……..…….
S.L.P……………………….……….…
……………………………..……..…….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAKITA, HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA, MKOA WA RUVUMA, MWAKA 2023/2024.**

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka **2023/2024.** katika shule hii Tahasusi ya ………… Tahasusi zilizopo shule hii ni ***CBG*** na ***HGL***.

Walimu, wafanyakazi, wanafunzi wenzako na wanajumuiya wote kwa ujumla wapo tayari kukupa kila msaada utakaohitaji pale itakapolazimika.

Shule ya Sekondari Makita ipo umbali wa **kilomita moja (1km)** kutoka kituo cha mabasi cha Halmashauri ya mji wa Mbinga, kandokando ya barabara iendayo Mbamba – bay. Usafiri ni wa pikipiki (Bodaboda) nauli ni **shilingi 1,000/=** na Tax nauli **shilingi 3,000/=.**

Muhula wa masomo kwa mwaka **2023/2024** unaanza tarehe **13/08/2023 , .** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **12/08/2023.** mwisho wa kuripoti tarehe 30/08/2023 kwa muhula wa kwanza wa masomo, unatakiwa kufika shuleni tarehe tajwa hapo juu. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti basi atakuwa amepoteza nafasi hii..

“ ***Tafadhali kama umepata shule nyingine na hutaripoti, toa taarifa hapa shuleni kwa barua ili Wizara ifanye utaratibu wa kumpa nafasi mwanafunzi mwingine***. ***Aidha baada ya miezi mitatu toka tarehe ya kuripoti shule, kama utakuwa hujafika shuleni basi Wizara itafanya utaratibu wa kujaza nafasi hiyo, nawe utakuwa umepoteza nafasi yako”***.

Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu zote husika kwa ukamilifu na kuzirejesha hapa shuleni, siku atakayoripoti. Asipokamilisha taratibu zote zilizoandikwa **HATAPOKELEWA.**

Motto wa Shule “ **ENTER TO LEARN, LEAVE TO SERVE”**

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu namba 1,2,3,4,5,6,7 na 8.

Mwisho ninakutakia mafanikio mema hapa shuleni.

**………………..**
**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**

*FOMU NA.1*

**MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.**

**1.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 SARE ZA SHULE:**

**(i). Sare za Darasani.**

a) Suruali mbili (02) **"Dark blue" –** (Ona kitambaa kimeambatishwa). ***Mshono:*** iwe na marinda mawili na upana wa chini iwe inchi 16, pia iwe na mkunjo chini, ukunjwe kwa nje (iwe na "turnup") inchi moja (01) na si vinginevyo.
**NB:** Tunashauri suruali ya kushona ndio nzuri kuliko ya mtumba / dukani.

b) Shati mbili (02) nyeupe ( tetroni) mikono mirefu.

c) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (02) vya kufunga na kamba (***gidamu)*** vyenye visigino vifupi.

d) Jozi mbili (02) za soksi au zaidi rangi nyeusi.

***e)*** Mkanda mweusi wa kuvalia suruali (***usiwe na urembo, pia chuma kinene kupita kiasi)***

f) Sweta rangi ya **"Dark blue"** yenye shingo ya **"V"** isiyopasuliwa mbele.

g) Tai mbili (02) za "**Dark blue"** rangi moja na suruali.

h) Nguo za kushindia ni suruali nyeusi na T – shirt rangi nyekundu (***isiyo na maandishi/picha wala kola).*** Asije na mavazi mengine tofauti na yaliyoagizwa.

i) Vesti nyeupe mbili )02)

j) Vijana wa kiislamu waje na **KANZU NYEUPE** ya kuvaa Msikitini siku ya Ijumaa na siku za sikukuu za kiislamu.

k) Aje na T – shirt moja yenye kola (***Aina ya Form six***) rangi ya blue isiyokuwa na maandishi yoyote. pia T-sirt hii anaweza nunua hapa shuleni kwa Shilingi 15,000/=, atavaa darasani siku atakazoelekezwa na akitoka nje ya shule.

l) Ni lazima kila mwanafunzi aje ya BARAKOA (MASK) mbili (02) ya rangi suruali "Dark Blue" kwaajili ya kujikinga na homa ya Corona (COVD-19)

**(ii). Vifaa vya Darasani.**

a) Daftari za kutosha (***Counter Books Quires 4***), Wanafunzi wa Sayansi (**CBG**) Counter books ***kumi (10),*** na wale wanaochukua masomo ya sanaa (**HGL**) Counter books ***saba (07).***

b) Kalamu ( ***blue pen or black pen***) za kutosha.

c) Penseli

d) Scientific calculator (***kikokotozi***) kwa wanafunzi wa sayansi (***function fx – 991 MS)***

e) Dissecting kits ( ***wanaochukua Biology***) zitakaguliwa siku ya kuripoti.

f) Saa ya mkononi

g) Graph paper pad, kwa matumizi yake darasani.

h) Mkebe (***Mathematical set***)

i) Koti la Maabara (***Lab.Coat***) rangi nyeupe mikono mirefu lipite magoti kwa wanafunzi wa Sayansi. (***Watavaa wakiwa Maabara tu***).

j) Bunda mbili za karatasi (***Ream A4***), hii ni kwa matumizi yake darasani.

k) Vitabu vya masomo husika (***Orodha imeambatanishwa kwenye Fomu Na.8***)

l) Faili mbili (02) kwa ajili ya kuhifadhia mitihani na kumbukumbu zingine "***Folder file"***

m) Taa ya Betri kwa tahadhari ya umeme ukikatika (ISIWE YA KUCHAJI KWA KUTUMIA UMEME) itumie betri au mionzi ya jua.

**(iii). Vifaa vya Bwenini.**

a) Ndoo mbili (02) za lita kumi (10) zenye mifuniko kwa matumizi ya mwanafunzi.
b) Godoro moja (01) futi 2 ½ kwa sita.
c) Mto mmoja (01) na foronya rangi ya blue bahari.
d) Shuka mbili (02) rangi ya blue bahari
e) Blanketi moja (01).
f) Chandarua moja (01)
g) Taulo
h) Ndala
i) Mswaki na dawa ya mswaki
j) Dumu la kuhifadhi maji ya kunywa moja (01) lita tatu (03) au lita tano (05) lenye rangi nyeupe **- Litakaguliwa**
k) Sanduku (***Trunker***) imara la bati moja lenye makufulu kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.

VCBG
i)Jembe lenye mpini moja (01).
ii)Mopa (***Draya***) mbili (02) zenye mpini.
iii)Brashi ngumu (***Hard broom***) moja (01) yenye mpini
iv. fagio laini soft broom moja

VHGL
i)Fagio laini la kufagilia ndani (***Soft broom***)
ii)Fyekeo moja(01)
iii)Mopa (***Draya***) mbili (02) zenye mpini
iv. jembe lenye mpini moja

**(iv). Vifaa vya bwaloni.**

a) Kikombe – 01
b) Sahani – 01
c) Bakuli – 01
d) Kijiko – 01

**(v). Sare za michezo.**

Mwanafunzi aje na **bukta moja** na **T – shirt** (***Jezi – 01***) moja ya michezo kwa mchanganuo wa rangi kama ifuatavyo;-

a) HGL – Jezi nyeusi, mistari myeupe
b) CBG – Jezi ya blue mistari myeupe
c) Wanafunzi wa **HGL** na **CBG** wote waje na **Tracksuit nzito nyeusi moja (01)** yenye mistari myeupe pembeni na isiwe na kofia kichwani (***yenye kola***).

**MAHITAJI BINAFSI:**

- Aje na fedha za kumtosha kwa ajili ya matumizi yake binafsi akiwa hapa shuleni.
- Vifaa vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa katika ofisi ya usajili kabla ya mwanafunzi kusajiliwa.
- Vifaa vya shule na mahitaji binafsi vinaweza kununuliwa kwenye duka lililoko shuleni.
- Masomo yanayofundishwa (A’Level) ni;-
  i. HISTORY

ii. ENGLISH
iii. GEOGRAPHY
iv. CHEMISTRY
v. BIOLOGY
vi. BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM)
vii. GENERAL STUDY (G.S)

**(vi). Ada na michango mbalimbali ya shule.**

**JEDWALI LA AINISHO LA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA TANO NA SITA.**

| S/N | MCHANGO | KIDATO CHA TANO |
|---|---|---|
| 01 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 02 | Mchango wa tahadhari | 5,000/= |
| 03 | Kitambulisho na Picha | 5,000/= |
| 04 | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| **05** | **JUMLA KUU** | **80,000/=** |

***ANGALIZO:*** (i). Ada ya mtihani wa Taifa **(NECTA)** kwa kidato cha sita, italipwa kulingana na maelekezo ya viwango vya wakati huo kutoka mamlaka husika.
(ii). Jumla ya Ada na michango mingine kwa kidato cha tano ni shilingi **188,000/=** Kwa kidato cha tano.

**(vi).Utaratibu wa kulipa.**

Ada **shilingi 70,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa kiasi cha **shilingi 35,000/=** kwa muhula au kulipa yote mara moja.

Shule haipokei fedha taslimu au hundi kutoka kwa wazazi/walezi wa wanafunzi na badala yake malipo yote yalioyoaninishwa kwenye jedwali hapo juu yalipwe kupitia **BENKI YA NMB** (***National Microfinace Bank***) kwenye tawi lolote Tanzania lililopo karibu nawe kabla ya kuja shuleni.
Jina la Akaunti ya shule; **MAKITA SECONDARY SCHOOL RECCURRENT ACCOUNT**, **Namba ya Akaunti ni 61701200113**

Baada ya kulipa hiyo michango Benki utapewa **BPS** (***Bank pay in slip***), kisha tuletee hiyo risiti shuleni kwa uthibitisho zaidi.

**……………………………..**
**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**

*FOMU NA. 2*

**SHERIA ZA SHULE:**

2.1 Shule inaendeshwa kwa **mujibu wa sheria ya Elimu Na.25** ya **mwaka 1978**, na kama ilivyorekebishwa **kwa sheria Na.10** ya **mwaka 1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu Nchini na **Ofisi ya Rais – TAMISEMI**, yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa, kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini saa 1.00 asubuhi.
c) Kuhudhuria shuleni siku zote na muda wote wa masomo.
d) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwemo vipindi vya dini kila wiki.
e) Kuhudhuria kazi zote za mikono.
***f)*** Kuhudhuria mikutano ya shule; ***<u>mfano</u>:- Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, vikao vya madarasani*** na vikundi mbalimbali vinavyotambulika kisheria; ***<u>mfano:-</u> Vilabu vya masomo, Dini, Utamaduni, maadili n.k.***
g) Kuitika miito ya dharula mara moja.
h) Kushiriki kuimba wimbo wa Taifa wakati wa kupandisha Bendera ya Taifa.
***i)*** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ( ***Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, ndevu na nywele ndefu au kunyoa kipara).***
j) Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni (Preparation) kuanzia saa 07:30PM hadi saa 10:30PM.
k) Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule. ***Mfano***; Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu, ***kwenda Posta***, ***Kanisan***i, ***Msikitin***i, ***Benki, Hospitali, Likizo*** au kwa shughuli yoyote itakayokulazimu kwenda nje ya shule.
l) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote (***Uwe mahali sahihi kwa wakati sahihi***).
m) Kutunza mali ya umma ***( Ukiharibu utagharimia***).
n) Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki **SIMU** ya mkononi ,**LAINI** ya simu ya mkononi au CHAJI ya simu ya mkononi na endapo ataonekana kumiliki vitu tajwa hapo juu **mwanafunzi atafutwa shule** .
o) Kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako wa shule, maana yake ni kukataa kuwa mwanafunzi wa shule hii.
p) Kuchochea au kusababisha mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku na haramu.
q) Kuvaa nguo za mtindo. ***Mfano***;**- Model.**
r) Wageni wa mwanafunzi wataruhusiwa kuonana naye baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu.
s) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufukuzwa shule.
t) Mwanafunzi atafuata maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
u) Hairuhusiwi mwanafunzi yeyote kwenda katika nyumba za walimu bila ruhusa kutoka kwa mwalimu.
v) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa wakati akiwa bado mwanafunzi; akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi awapo mwanafunzi.
w) Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu na atapaswa kuwa na kibali (***Get pass***) cha maandishi.
x) Ni marufuku kuvaa/ kuja na mavazi kinyume na yale yaliyoagizwa
y) Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki kamera au komputa mpakato (LAPTOP) Shuleni.

***NB: " Shule haitavumilia mwanafunzi atakayekiuka kanuni hizo hapo juu"***

***MUHIMU:***

***1. mwanafunzi hupaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na HAKUNA mtumishi anaruhuswa kutunza simu ya mwanafunz***

***2. Mwanafunzi awapo shulen anatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumiwa na mwanafunzi mmoja***

**3. mwanafunz ataruhuswa kurudi nyumban kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule (msiba au ugonjwa)**

**2.2 Makosa yafuatayo yatasababisha ufukuzwe shule.**

a) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.
b) Wizi
c) Mwanafunzi kumiliki **SIMU YA MKONONI** au **LAINI YA SIMU** ya mkononi.
d) Kushirikiana kuendeleza imani za kishirikina
e) Kunyanyapaa na uonevu wa aina yoyote.
f) Kukataa adhabu kwa makusudi.
g) Kuoa
h) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
i) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, uvutaji sigara na biashara ya madawa yote ya kulevya.
j) Makosa mengine ya jinai
k) Kogoma na kuhamasisha mgomo.
l) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
m) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
n) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
o) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
p) Kushiriki matendo ya uharifu, na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
q) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana ndani na nje ya shule
r) Kujiachisha shule mwenyewe.
s) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, dawa n.k.
t) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
u) Kufuga ndevu.

*FOMU NA. 3*

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI.**

**A: MWANAFUNZI.**

1. Jina kamili (***Matatu***): …………………………………………………………………
2. Shule ya Sekondari aliyosoma (***O'Level***): ……………………………………………
3. Namba ya Mtihani: ………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa: ……………………………………………………………………...
5. Nakubali nafasi niliyopewa / Siikubali, apewe mwingine (***Kata neno lisilohusika***).
6. Nakiri / naahidi nitajibidisha katika Taaluma, Nidhamu, Elimu ya kujitegemea na michezo, pia kutomiliki simu au Laini; wala chombo kinachotumia umeme shuleni, kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai kama ilivyoainishwa katika sheria za shule
7. Sahihi: ……………………………….. Tarehe: ………………………………

**B: MZAZI / MLEZI.**

Mimi ………………………………………mzazi/ mlezi wa …………………………… nimesoma kwa makini maagizo ya mwanangu kujiunga na shule ya Sekondari Makita; Naahidi kumtimizia mwanangu maagizo yote na pia nitashirikiana na walimu katika kumlea mwanangu kinidhamu ili apate Taaluma inayokubalika na endapo nitazembea nihesabiwe kuwa nimegoma kumpa malezi mwanangu na nichukuliwe hatua zinazostahili.

Jina la Mzazi/Mlezi: ……………………………………………………………………
Anuani: ……………………………………………………………………………………..
Kijiji / Mtaa: ………………………………………………………………………………..
Sahihi ya Mzazi / Mlezi: …………………………………………………………………..
Namba ya simu: ……………………………………………………………………………
Tarehe: ……………………………………………………………………………………..

**C: AFISA MTENDAJI KATA/KIJIJI/MTAA.**

Jina: ………………………………………………………………………………………...
Kijiji / Kata: ……………………….. Wilaya: ………………… Mkoa: ……………………
Nathibitisha kuwa mwanafunzi …………………………….. ni wa kijiji / kata hii na raia wa Tanzania / si raia wa Tanzania.

Sahihi: …………………… Muhuri: ……………… Tarehe: …………………….

**…………….**
**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**

*FOMU NA. 4*

**A: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (*Ijazwe na mwanafunzi*)**

1. Jina la mwanafunzi (*Matatu*)***:*** ………………………………………………………
2. Kidato cha ………………………….. Tahasusi ya ………………………………..
3. Mahali ulipozaliwa: ………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa: ………………………………………………………………
5. Jinsia: ……………………………………………………………………………..
6. Umri: ……………………………………………………………………………..
7. Anwani ya nyumbani: ……………………………………………………………
8. Anwani ya Mzazi/Mlezi (*kama tofauti na hiyo hapo juu*)…………………………..
9. Jina la Mzazi/Mlezi: ……………………………………………………………....
10. Dini: ………………………………………………………………………………
11. Kidato ulichopokelewa: …………………………………………………………..
12. Shule ya Sekondari uliyomaliza: …………………………………………………
13. Shule ya Msingi uliyomaliza darasa la saba: ……………………………………..
14. Shughuli unazopendelea mbali na masomo, kwa mfano: Mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, unaimba n.k ……………………………………………………………..
15. Wilaya unayotoka: ………………………………………………………………..
16. Mtaa: ……………………………….. Kata: ……………………………………
17. Nikihama nitatoa taarifa: …………………………………………………………
18. Mimi ……………………………………………nakiri taarifa nilizotoa ni sahihi.

Sahihi ya Mwanafunzi: …………………………Tarehe: …………………………

*NB: ENDAPO MWANAFUNZI ATATOA TAARIFA ZISIZOSAHIHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KINIDHAMU.*

**B: AFISA MTENDAJI KATA/KIJIJI/MTAA.**

Jina: ……………………………………………………………………………………..
Kijiji / Kata: ……………………….. Wilaya: ………………… Mkoa: ……………………
Nathibisha kuwa mwanafunzi …………………………….. ni wa kijiji / kata hii na raia wa Tanzania / si raia wa Tanzania.

Sahihi: …………………… Muhuri: ……………… Tarehe: …………………….

**…………….**
**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**

*FOMU NA. 5*

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**(*FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA*)**

**PART A:** Date:…………………………

FROM.………………………..
………………………………..
………………………………..

TO: REGIONAL/DISTRICT MEDICAL OFFICER,
P.O BOX ……………
……………………….

Mr/Mrs/Miss ……………………………….. Age: ……… Sex: ……….. Height: ……….
*(Name in full)*

Pleased examine the above named as to his physical and mental fitness for a full – time, Advanced Level of Secondary Education studies.
The Examination should include the following ineligible in case of a defect.

1. (a). Eye – sight……………………….
   (b). Hearing (Ears)…………………...
   (c). Limbs……………………………
   (d). Speech…………………………...
   (e). Venereal disease…………………
   (f). Stool Examination……………….
   (g). TB test……………………………
   (h). Spleen
   (i). Abdomen…………………………
   (j). Urine for plamotest………………
   (k). Syphilis test………………………
   (l). Blood group………………………
   (m). Blood count(Red & white)……….
   (n). Epilepsy…………………………..
   (o). Leprosy…………………………...
2. Neurons
3. Other serious disease

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**

*(To be completed by government Medical Officer)*

I have examined the above – named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for full – time student.

1. (a). Eye – sight……………………………..
   (b). Hearing (Ears)………………….............
   (c). Limbs………………………………….
   (d). Speech………………………….............
   (e). Venereal disease……………………….
   (f). Stool Examination…………………….
   (g). TB test………………………………….
   (h). Spleen………………………………….
   (i). Abdomen……………………………………..
   (j). Urine for plamotest…………………………
   (k). Syphilis test…………………………………
   (l). Blood group…………………………………
   (m). Blood count(Red & white)…………………..
   (n). Epilepsy………………………………………
   (o). Leprosy…………………………......................
2. Neurons
3. Other serious disease

**ADDITIONAL INFORMATION**

If any e.g physical impairments infection, chronic or family disease …………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………………………………………….

*I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION*.
Station: …………………………………………..

Name: ………………………………………… Signature: …………………………..

Date: ………………………….. Designation: ……………………………………….

Official stamp: ………………………………….

*FOMU NA. 6*

**TAARIFA ZA NDUGU WATAKAOFIKA KUMUONA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI ZA MWANAFUNZI.**

**A: JEDWALI LINALOONYESHA NDUGU WA MWANAFUNZI NA PICHA ZAO ZIWEKWE HAPO CHINI.**

| Na | Jina | Jinsi | Anwani yake | Uhusiano | Kabila | Anakotoka | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | | | | |
| 02 | | | | | | | |
| 03 | | | | | | | |
| 04 | | | | | | | |

Habari nyinginezo:
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi: ………………………….. Tarehe: …………………………..

**B: MZAZI AWAIDHINISHE HAO NDUGU WA MWANAFUNZI.**

Mimi …………………………………… Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi …………………….. Ninawaidhinisha watajwa hapo juu kuwa ni ndugu wa mwanangu na watakuwa wakifika kumwona na kusikiliza shida mbalimbali wakati ambao mimi kama Mzazi/Mlezi nitakuwa nimeshindwa kufika.

Sahihi: …………………….. Namba ya simu: …………………….. Tarehe: …………….

**C: KIONGOZI WA SERIKALI YA MTAA/KIJIJI ATHIBITISHE TAARIFA HII.**

Mimi …………………………………. Cheo …………………………… Kijiji/Mtaa……… Nathibitisha kuwa watajwa hapo juu wameteuliwa na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi …………………………na ninakuomba uwapokee wawe walezi mbadala wa mwanafunzi tajwa hapo juu.

Sahihi: ……………………….. Mhuri: ………………. Tarehe: ………………..

Namba ya simu: …………………………….

*FOMU NA. 7*

## AHADI/KIAPO CHA MWANAFUNZI.

Mimi ……………………………………………………Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI MAKITA KIDATO CHA TANO**, mchepuo wa ……………. Mwaka 2018, ninaipokea na kuikubali nafasi niliyopewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya **Sekondari Bweni – MAKITA.** Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia.

Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni;-

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyochaguliwa kusoma.
ii. Nitajishusha na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma, na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita Mzazi/Mlezi wangu …………………………… (***Jina la Mzazi***) kwa ajili ya hatua zaidi.

Sahihi ya Mwanafunzi: ……………………….. Tarehe: ………………..

…………………

**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**

*FOMU NA. 8*

**VITABU VYA MASOMO HUSIKA.**

**A: HISTORY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Major issue in Africa ICD | |
| 02 | Major events in Africa History | Mwajage |
| 03 | Europe from 1815 by Peacock | |
| 04 | How Europe under developed Africa | Walter Rodney |
| 05 | African since 1800 4 Edition | By Roland Oliver Atmore |
| 06 | The political Economy Imperialism | By Nabudere |
| 07 | Advanced level History for form five and six | Oxford |
| 08 | Advanced level History (Paper 1 & 2) | By Z. Kamili |
| 09 | Essential hstory A LEVEL paper 1 and 2 | Salehe Yassn |

**B: GEOGRAPHY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Fundamental Geography | By Josephat Mwita, A.M |
| 02 | Principles in physical Geography | By Monk House |
| 03 | Practical Geography for Africa | By John Richard |
| 04 | Photography Interpretation and elementary surveying for secondary level new edition | By S.E. Dura |
| 05 | Regional Geography | By Nyambari Nyangwine |
| 06 | General Geography in diagrams | By R.B Bunet |
| 07 | Practical geography for east afrca | Pritchard FJ |

**C: ENGLISH PAPER 1 & 2**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Contemporary English for Advanced level | By Francis Myawi |
| 02 | New Advanced level English | By Charles |
| 03 | English for Form five and six | Michael Kadege |
| 04 | A complete English course for form six | Michael Kadege |
| 05 | Advanced Learner Dictionary | Oxford |
| 06 | Teaching English as a foreign Language | G. Broughton et al |
| 07 | Longman English Grammar | L.G. Alexander |
| | **PAPER 3** | |
| 1 | **NOVELS:**<br>a) The beautiful one not yet born<br>b) A grain of wheat<br>c) A man of the people<br>d) Vanishing shadow | <br>A.K Amah<br>Ngugi Wathiongo<br>Chinua Achebe<br>N. Kayombo |
| 2 | **POETRY:**<br>a) Selected poems from Institute of Education | |

**D: CHEMISTRY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Organic chemistry part A & B | Mzumbe book project |
| 02 | A' level chemistry, 4th Edition | E.N. Ramsden |
| 03 | Conceptual chemistry, class, XI & XII | By S. Chand |
| 04 | Chemistry for A' level and 1st year undergraduate students inorganic chemistry part A & B | By J.S Maro and Mikese Walla) Mzumbe book project |
| 05 | Advanced level physical chemistry with general chemistry | Ape Network |

**E: BIOLOGY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Biological science 1st & 2nd Ed | |
| 02 | Guidance to dissection | |
| 03 | Dissecting kit | |
| 04 | Understanding Biology 1st ed. | C.J Legg with Macklean |

## MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHA SHULENI

i. Cheti cha kuzaliwa
ii. Result slip
iii. Picha (**Passport size) nne (04**) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
iv. Picha **(passport size ) mbili (02**) za mwanafunzi.
v. Aje na kadi ya **BIMA YA AFYA YA TAIFA (NHIF**) kwa ajili ya matibabu; ni lazima kwa kila mmoja. Mzazi /Mlezi hakikisha kwamba umemkatia mwanao **kadi ya Bima ya Afya (NHIF**).

**NB:** Endapo mwanafunzi hana kadi ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) alipie kiasi cha shilingi elfu tano (5,000/=) kwa ajili ya Bima ya Afya kikaya (CHF), kama jedwali la michango linavyoelekeza, fedha hiyo ilipwe kwenye Akaunti ya Ada na michango mingine kisha aje na risti ya malipo ya Benki (BPS)

**“ KARIBU SANA MAKITA SEKONDARI “**

**…………………**
**EMMANUEL S MWAMASIKA**
**MKUU WA SHULE**